

## **Ripoti ya Mkutano wa Nairobi**

**4-7/07/09**

Imeandikwa na Filbert Mbecha

Mkutano ulijumuisha jumla ya vyama visivyo vya kiserikali kumi na mbili, kutoka mchi mbali mbali Afrika, ikiwemo Tanzania, Ghana, Kenya, Uganda, South Africa, Egypt, Botswana, Rwanda, Burkina Faso na Netherlands, ambao walifadhili mkutano huo chini shirika lijulikanalo kama Interface for Cycling Expertise (I-CE).

4/07/09

Tulifanya msafara wa baisikeli kwa washiliki wote, wenye umbali wa 100km, kutoka Nairobi hadi ziwa Magadi, na kurudi kwa gari. Na kwa kila mshiriki alipewa cheti cha kushiriki.

5/07/09

Tulianza mkutano katika mji wa Naivasha, ambao upo katika ziwa Naivasha. Kwanza tulianza kutambulishana na kufanya michezo ya kuchangamshana ili kuweza kufahamiana majina kwa urahisi ulio ongozwa na Moses John Kibera katibu wa Chama cha Uvumbuzi kilichopo Kenya.

6/07/09, 7/07/09

Tulianza mkutano rasmi: Tulichagua jina la mtandao kuwa ni African Bicycle Network, ni jina lililochaguliwa kati ya majina yaliyopendekezwa.

Baada ya hilo mwenyekiti alitoa nafasi kwa kila mshirik kutoa tamko ya kwamba nini anategemea kupata iwapo tutaunda huu mtandao. Kati ya hayo ikiwemo yafuatayo:

- Tutaondoa fikra potofu za watu katika jamii kwamba baisikeli ni usafiri wa mtu masikini.
- Utakuwa umetuweka katika hali ya kuwa marafiki kwa nchi zote za Afrika na kushirinana
- Uttufanya kuwa na mwonekano zaidi usafiri wa baisikeli Afrika nzima tofauti na hivi sasa
- Tutafaidika kiuchumi, kwa sababu tutaweza kuagiza baisikeli kwa wingi na kuziua kwa gharama nafuu

Baada ya kuchangia hayo baadhi, tuliweza kuangalia ni kwa jinsi gani tutafanikiwa:

- Malengo (objectives)
- Mtano wetu (vision)
- Ni kwa jinsi gani tutafanikisha (mission)

Tulijigawa katika makundi manne na kila kundi kuchangia kuhusu hayo matatu:

Malengo (objectives)

- Kushirikiana katika kupeana taarifa mbali mbali na uzoefu ulio mzuri miongoni mwa wanamtandao.
- Kuzihamasisha jumuiya zote pamoja kuweza kuwa na sera ya kitaifa yenye kuhamasisha baisikeli kuweza kuwa na mwonekano

- Kuzipa nguvu (msukumo) Jumuiya kuweza kupiga hatua kiuchumi katika maisha kupitia baisikeli
- Kuimarisha taarifa zetu, kutoa ujuzi na uzoefu kwa kuhamasisha watunga sera mbali mbali kuwa baisikeli inatunza mazingira na kuyaendeleza kwa kutotoa moshi.
- Kutetea na kuhamasisha usafiri usiotumia mafuta (NMT) kuwa ni suala la kuwekewa kipaumbele zaidi

#### Mtazamo (Vision)

- Kuwa marafiki kwa wapanda baisikeli wote Afrika
- Kuwa na jambo la pamoja katika mtandao ambalo litalenga kutetea na kfaunay mchakato wa pamoja wa aina ya baisikeli tunazohitaji kulingana na mahitaji ya sehemu husika
- Mpanda baisikeli aweza kusaminiwa
- Wapanda baisikeli kuwa ndio watetezi wakuu wa utunzaji wa mazingira Afrika

#### Jinsi ya kufanikisha (Mission)

- Kwa kuhahasisha baisikeli kuwa ni chombo cha usafiri, kupitia sera zetu na taarifa
- Kwa kutoa umuhimu na faida ya baisikeli kiafya, kiuchumi na kwa utunzaji wa mazingira kwa jamii
- Kujifunza kutoka katika vyama vingine ili kupeana uzoefu wa utendaji kupitia mtandao
- Kutoa mahitaji ya pamoja na kuongeza ubora wa maisha ya wetu wan chi zote za Afrika kipita baisikeli, usafiri usiotumia mafuta
- Kupitia mtandao wa Afrika kwa kuhamasisha jamii zote kutumia baisikeli na kupa msukumo wenye nguvu

#### Kazi za Mtandao

- Kukusanya taarifa kutoka vyama vyote vya kijamii kupitia email na website / barua pepe na tovuti)
- Kuzijengea uwezo vyote Afrika
- Kuunganisha matukio ya msafara, kutoka vyama mbali mbali, na mikutano ili kuimarisha mtandao
- Kuimarisha shughuli za website na uchapishaji wa maelekezo yanayohusu mtandao na makongamano ya mwaka kutoka vyama mbali mbali vya kijamii
- Kufanya makubaliano ya msafara ya baisikeli ambayo itahusisha vyama vyote kutoka nchi moja hadi nyingine

#### Hard

itaingiza bidhaa (input), itasambaza (distribution) na kuwa na uundaji katika karakana (factory)

## Soft

- Kutunza taarifa (documentation)
- Kutoa taarifa katika vyombo vya habari (media)
- Kuandaa data na kuzitoa (prepare data and link)
- Kuwa na rasilimali (fundraising)
- Kutunza taarifa (database experts)
- Kutoa elimu na mafunzo (training/education)
- Kufaidika na kuhamasisha (advantage and lobby)

Kuwa na katiba ya mtandao (network constitution) ambayo itasaidia kulinda kanuni ya mtandao.